BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI NA TISA

Kikao cha Kumi na Mbili – Tarehe 20 Mei, 2025

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

### Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale kwa mwaka 2025/2026.

### Mwenyekiti wa Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo:

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale kwa mwaka 2025/2026.

## II. MASWALI:

### Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

247. MHESHIMIWA MUSSA FOUM MUSSA (Jimbo la Kiwani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo ya Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

Tunamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia nchi yetu kuendelea kuwa na amani na usalama. Hata hivyo, nchi yetu inakabiliwa na Uchaguzi Mkuu ambao kikawaida hujitokeza matokeo yanayoashiria uvunjifu wa usalama na amani yetu.

Je, Serikali inawahakikishia vipi wananchi wake juu ya usalama wao wakati na baada ya uchaguzi huo.

**Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais:**

207. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais:

(a) Ni upi muarubaini wa tatizo la ongezeko la matumizi ya madawa ya kulevya na uraibu.

(b) Serikali inachukua jitihada zipi kuinusuru jinsia ya kinamama vijana inayoonekana kushamiri ongezeko lake kwa siku za hivi karibuni.

**Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:**

216. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

Kwa kiasi gani suala la Haki za Binadamu linatekelezwa katika Vyuo vyetu vya Mafunzo vilivyopo nchini.

**Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:**

126. MHESHIMIWA BAHATI KHAMIS KOMBO (Jimbo la Chambani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga kituo cha Zimamoto kutoka Barabara ya Ole – Kengeja.

**Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:**

115. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

Kwa kuwa nishati mbadala ya mitungi ya gesi ndio suluhisho la matumizi ya nishati ya kuni na mkaa.

Je, kuna utaratibu upi wa Wizara ya Uwezeshaji wa kuwasaidia wajasiriamali wanaotengeneza maseredani ya mkaa katika eneo la Mwanakwerekwe kupata ajira mbadala.

**Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:**

4. MHESHIMIWA FATMA RAMADHAN MOHAMMED (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

   Kuna mpango gani wa Serikali utakaohakikisha uhaba wa vitendea kazi vya usafiri unatatuliwa kwa upande wa Pemba, hasa ikizingatiwa kuwa, uhaba huo unazorotesha utendaji wa kazi wa Afisi nyingi za Serikali.

**Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:**

20. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:

    Wizara yako iliulizwa swali katika Mkutano wa 15 wa Baraza la Wawakilishi, kuhusiana na malalamiko ya wananchi 200 wa kijiji cha Daya, jimbo la Mtambwe walioomba viwanja katika shamba la Serikali liliopo eneo la "Daya kwa Mjinga", na hatimae shamba hilo alipatiwa ndugu Rashid Ali ambae ameanza kukata viwanja na kuuza bila ya kufuata taratibu, huku Serikali ikiahidi kulifuatilia suala hili kupitia Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo.

    (a) Serikali imefikia wapi katika kulifuatilia suala hilo.

    (b) Je, kuna majibu gani ambayo Serikali ingeyatoa kwa wananchi wa jimbo la Mtambwe.

    (c) Serikali inawasaidia vipi wananchi hawa ambao wengi hawana maeneo ya kujenga na bado wanayo mahitaji makubwa ya kujipatia kipato.

**Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:**

112. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

     Ni lini ahadi ya kukikarabati kiwanja cha Nyarugusu itatekelezwa ili kiweze kutumika katika shughuli mbali mbali za Serikali na za kijamii.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

66. MHESHIMIWA CHUMU KOMBO KHAMIS (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

    Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Mwinyi ameifungua Pemba katika nyanja tofauti zikiwemo barabara na usafiri wa anga ili kuendeleza utalii katika kisiwa hicho.

    Je, Serikali ina mpango gani katika kuendeleza ujenzi wa viwanja vya ndege kisiwani humo.

**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

97. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

    Kitafiti nazi za Zanzibar zinaonesha kuwa zina madini ya protini salama ya kutosha kwa afya ya mlaji. Je, kwa kiasi gani kampeni ya kurejesha minazi mirefu inaweza kuwa na tija katika kurejesha zao la nazi Zanzibar.

**Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:**

280. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

     Je, Serikali inawatumia vipi waandishi wa habari hapa nchini katika kuutangaza utalii wetu.

## III. HOJA ZA SERIKALI:

**Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:**

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale kwa mwaka 2025/2026.

Zanzibar,
20 Mei, 2025.

(Raya Issa Msellem)
**KATIBU WA BARAZA**